

Uongo dhidi ya Ukweli Chanjo ya COVID-19

Uongo: Chanjo za COVID-19 si salama.

UKWELI: Chanjo za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi.

Usalama ni kipaumbele cha kwanza cha [mchakato wa uundaji na uidhinishaji wa chanjo nchini Marekani](#). Mchakato wa uundaji wa chanjo za COVID-19 ulihusisha hatua kadhaa zinazolingana na zile zinazotumiwa kuunda chanjo zingine kama vile chanjo ya mafua au surua, ambazo zimefanikiwa kuwalinda mamilioni ya wakazi wa jimbo la Ohio kwa miongo kadhaa. Mamlaka ya Kudhibiti Chakula na Dawa (FDA) ya Marekani, pia wataalamu huria wa matibabu, wamehakikisha kuwa kila kipengele cha chanjo za COVID-19 kimechunguzwa kwa undani na kikamilifu. Ushahidi unaonyesha kuwa chanjo za COVID-19 ni salama na hufanya kazi kuzuia COVID-19. Mojawapo ya chanjo mbili ambazo zinatumia idhini ya FDA ya kutumiwa wakati wa dharura [chanjo iliyotengenezwa na Pfizer-BioNTech ilikuwa na ufansi wa 95%](#), na [chanjo iliyotengenezwa na Moderna ilikuwa na ufansi wa 94%](#) katika tafiti za kimatibabu zenye awamu 3 zilizohusisha zaidi ya washiriki 70,000 kati ya tafiti zote mbili. Ingawa chanjo za COVID-19 zenyewe zimetengenezwa hivi karibuni, teknolojia inayotumika katika chanjo za mRNA, kama zile zilizoundwa na Pfizer-BioNTech na Moderna zimefanyiwa utafiti kwa miongo kadhaa.

Uongo: Chanjo za COVID-19 ziliharakishwa na kuundwa kwa haraka sana.

UKWELI: Uundaji wa chanjo ya COVID-19 na tafiti za kimatibabu zilifanywa kwa ukamilifu, na kwa sababu ya juhudi ya kisayansi ya kimkakati ya kuboresha mchakato, zinaweza kuundwa kwa ufanisi zaidi.

Hakujakuwa na njia za mkato katika mchakato wa uundaji wa chanjo. Mchakato huo umeharakishwa zaidi [kufuatia juhudi za kimkakati](#) za kufanya awamu za majaribio zinazofanyika kwa wakati mmoja, na pia kujitolea kusaidia kupunguza wakati unaohitajika na kupunguza au kuondoa vipindi vya kusubiri vinavyochukua miezi ambapo hati zingetayarishwa au kuwa zinasubiri kupitiwa. Aidha, wakati wa uundaji wa chanjo, Maafisa Wakuu Watendaji wa AstraZeneca, BioNTech, GlaxoSmithKline, Johnson & Johnson, Merck, Moderna, Novavax, Pfizer, na Sanofi walitoa [ahadi ya kihistoria](#) kwa ulimwengu, wakitaja azimio la pamoja la kuzingatia uadilifu wa mchakato wa kisayansi huku wakifanya kazi wakiwa na nia ya kuwasilisha chanjo za kwanza za COVID-19 kwa mamlaka za udhibiti na uidhinishaji. RNA ya kupeleka ujumbe (mRNA), ambayo ilitumiwa kwenye chanjo mbili za kwanza katika kutuma ombi la idhini ya FDA kwa matumizi ya dharura (Pfizer-BioNTech na Moderna), ingawa ni mpya, inajulikana. Watafiti wamekuwa wakifanya utafiti kuhusu mRNA kwa miongo kadhaa, na tafiti za kimatibabu za awamu ya awali zinazotumia chanjo za mRNA zimefanywa kwa mafua, Zika, kichaa cha mbwa, na saitomegalovirusi (CMV). Maendeleo ya kiteknolojia ya hivi karibuni katika biolojia na kemia ya RNA na pia mifumo ya uwasilishaji, yamewezesha chanjo hizi za COVID-19 zinazotumia RNA kuundwa zikiwa chanjo salama na zenye ufanisi.

Uongo: Chanjo za COVID-19 zitakuwa za lazima kwa kila mkazi wa jimbo la Ohio.

UKWELI: Jimbo la Ohio halitafanya chanjo ya COVID-19 kuwa ya lazima.

Jimbo la Ohio halitamlazimisha mtu yeyote kupata chanjo ya COVID-19. Chanjo hiyo itapatikana kwa wakazi wote wa jimbo la Ohio watakaomua kuipokea, kadiri kiasi cha chanjo kinapongezeka.

Uongo: Unaweza kupata ugonjwa wa COVID-19 kutokana na chanjo za COVID-19.

Ukweli: Chanjo za COVID-19 hazitakupa ugonjwa wa COVID-19.

Hakuna chanjo yoyote ya COVID-19 kati ya zile zinazotengenezwa kwa sasa nchini Marekani ambazo hutumia virusi amilifu vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19. Chanjo za Pfizer-BioNTech na Moderna ni chanjo za asidi ya ribonyuklea inayowasilisha ujumbe, au mRNA. (Angalia hapa chini kwa ufafanuzi zaidi.) Lengo la chanjo za COVID-19 ni kufunza mifumo yetu ya kinga kutambua na kupigana dhidi ya virusi vinavyosababisha COVID-19. Wakati mwingine mchakato huu unaweza kusababisha athari zisizokusudiwa, kama vile uchovu, maumivu ya kichwa, uchungu au kubadilika kwa rangi ya mahali palipodungwa kuwa pekundu, na maumivu ya misuli au viungo. Dalili hizi ni za kawaida na ni ishara kuwa mwili unakuza kinga. Kwa kawaida huchukua wiki chache kwa mwili kukuza kinga baada ya chanjo, na baadhi ya chanjo huhitaji dozi mbili. Hiyo ina maana kuwa inawezekana kwa mtu kuambukizwa na virusi vinavyosababisha COVID-19 punde tu kabla ya, au baada ya, kupokea chanjo na kisha kugonjeka, kwa sababu chanjo hiyo huchukua muda kutoa kinga. Jifunze mengi kuhusu [jinsi chanjo za COVID-19 hufanya kazi](#).

Uongo: Chanjo zinazotumia DNA yangu au muundo vinasaba.

UKWELI: kupokea chanjo ya mRNA hakutabadilisha DNA yako.

Asidi ya ribonyuklia inayowasilisha ujumbe, au mRNA, haiwezi kubadilisha au kugeza muundo wa vinasaba (DNA) vya mtu. mRNA ya chanjo ya COVID-19 haiingii kwenye kiini cha seli, ambapo ndipo DNA huwekwa, na hivyo haiathiri au kuingiliana na DNA yako kwa njia yoyote ile. mRNA kutoka kwa chanjo za COVID-19 inaweza kufafanuliwa kwa urahisi zaidi kuwa maagizo ya mwili wako wa jinsi ya kutengeneza kipande cha "protini iliyochochongoka" ya kuwezesha mfumo wetu wa kinga kutambua kuwa protini hii haifai kuwa hapo na kuanza ushughulikiaji wa kinga na kutengeneza kingamwili. Kimsingi, chanjo za COVID-19 zinazotumia mRNA hufanya kazi na ulinzi asilia wa mwili ili kukuza kinga dhidi ya virusi, na kuzipa seli zako mwongozo wa jinsi ya kutengeneza kingamwili. Jifunze mengi kuhusu [jinsi chanjo za COVID-19 hufanya kazi](#).

Uongo: Ikiwa nimepona kutokana na ugonjwa wa COVID-19, sihitaji kupata chanjo ya COVID-19.

UKWELI: Watu waliopona kutokana na COVID-19 huenda wakanufaika kutokana na kupata chanjo.

Kwa wakati huu, wataalamu hawajui ni kwa muda gani mtu amelindwa dhidi ya kugonjeka tena baada ya kupona COVID-19. Kwa sababu ya hatari kali za kiafya zinazohusiana na COVID-19, na kwa sababu kuna uwezekano wa kuambukizwa tena COVID-19, watu huenda wakashauriwa kupata chanjo ya COVID-19 hata kama walikuwa wameugua COVID-19 hapo awali. Kinga ambayo mtu hupata kutokana na kuambukizwa, inayoitwa kinga asili, hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Kinga asili na kinga inayotolewa na chanjo ni vipengele muhimu vya COVID-19 ambavyo wataalam wanajaribu kujifunza mengi zaidi, na Vituo vya serikali kuu vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) vitajulishwa umma kadri ushahidi mpya unapopatikana.

Uongo: Ugonjwa wa COVID-19 si hatari sana, hivyo sihitaji kupokea chanjo.

UKWELI: Hatari ya dalili za COVID-19 hutofautiana pakubwa, na kupokea chanjo kunaweza kuzuia kuambukizwa COVID-19.

Ingawa watu wengi wenye COVID-19 huwa wakongjwa tu kiasi, wengine wanaweza kuwa [wagonjwa sana](#) au kufa. Hakuna mbinu ya kujua jinsi ugonjwa wa COVID-19 utakuathiri, hata kama hauko katika hatari [kubwa ya kupata matatizo mabaya zaidi](#). Vile vile, ukiugua COVID-19, huenda ukasambaza ugonjwa huo kwa marafiki, familia, na wengine walio karibu nawe ambao unapokuwa mgonjwa. Chanjo ya COVID-19 hukusaidia kukulinda kwa kuwezesha mwili wako kuunda kingamwili bila kuugua. Jifunze mengi kuhusu [jinsi chanjo za COVID-19 hufanya kazi](#).

Uongo: Utapata matokeo chanya ya kipimo cha virusi vya COVID-19 utakapopokea chanjo ya COVID-19.

UKWELI: Chanjo za COVID-19 hazitakufanya upate matokeo chanya ya vipimo vya COVID-19.

Chanjo ambazo zinatumika kwa sasa katika majaribio ya matibabu nchini Marekani hazitakufanya uwe na matokeo chanya kwa [vipimo vya virusi](#), ambavyo hutumika kubaini iwapo una maambukizi kwa sasa. Ikiwa mwili wako utaunda kingamwili, ambalo ndilo lengo la kupata chanjo, kuna uwezekano unaweza kupata matokeo chanya kwa baadhi ya [vipimo vya kingamwili](#). Vipimo vya kingamwili huonyesha kuwa ulikuwa na maambukizi ya hapo awali na kuwa huenda ukawa na kiwango fulani cha kinga dhidi ya virusi. Wataalamu kwa sasa wanachunguza jinsi chanjo ya COVID-19 huenda inaathiri matokeo ya vipimo vya kingamwili.

Uongo: Chanjo zingine, kama vile chanjo ya mafua, zitazuia COVID-19.

UKWELI: Ni chanjo tu zilizoundwa mahususi kuzuia COVID-19 zitakulinda dhidi ya COVID-19.

Chanjo zingine, kama vile zile za mafua, surua, au za magonjwa mengine, hazitakulinda dhidi ya COVID-19. Ni chanjo tu zilizoundwa mahususi kukulinda dhidi ya COVID-19, baada ya kuidhinishwa kwa matumizi na FDA, zinaweza kuizuia. Ingawa chanjo ya mafua haitakulinda usiugue COVID-19, inaweza kukulinda usipate mafua unapokuwa unaugua COVID-19

Uwongo: Hakutakuwa na chanjo za kutosha kwa kila mtu.

UKWELI: Huku utengenezaji wa chanjo ukiendelea kuongezeka, kila mkazi wa jimbo la Ohio anayetaka kupokea chanjo ataipata ili kuzuia COVID-19.

Mwanzoni, FDA itakapoidhinisha matumizi ya chanjo mahususi za COVID-19 nchini Marekani, kutakuwa na kiasi kidogo cha dozi kitakachopatikana. Jimbo la Ohio limejitolea kuhakikisha chanjo hiyo inpatikana kwa watu wote wanaotaka kuipokea, haraka iwekenavyo wakati chanjo hizo zitakapowasili Ohio. Baada ya muda, kadri utengenezaji wa chanjo unavyoongezeka na kiasi kikubwa kupatikana, kila mkazi wa jimbo la Ohio ambaye anataka kuchanjwa atafanya hivyo.

Uongo: Chanjo za COVID-19 zitapachika mikrochipu za kufuatilia watu.

UKWELI: Sindano za chanjo hazina mikrochipu za ufuatiliaji.

Hakuna sindano za chanjo au dawa zinazopuliziwa kwa pua - ikiwemo chanjo za COVID-19 - huwa na mikrochipu, nanochipu, vifaa vya ufuatiliaji vya RFID, au vifaa ambavyo vitafuatilia au kudhibiti mwili wako kwa njia yoyote. Kama ilivyo kawaida ya kufuatilia bidhaa yoyote inayosafirishwa, dozi za chanjo zitakazosafirishwa zitafuatiliwa zitakapokuwa zinasafirishwa na kupeanwa kote nchini. Hata hivyo, dhana kwamba chanjo hizi zina vifaa vya kufuatilia vitakavyopachikwa kwa wakazi wa Ohio si kweli.

Uwongo: Chanjo za COVID-19 husababisha utasa au matatizo mengine hatari ya kimatibabu.

UKWELI: Hakuna matatizo hatari ya usalama yameshuhudiwa kwa chanjo za COVID-19 ambazo zimeomba kuidhinishwa kwa matumizi ya dharura.

Katika [utafiti wa kimatibabu wa awamu ya 3 wa Pfizer-BioNTech](#) wa zaidi ya watu 43,000, na [utafiti wa kimatibabu wa awamu ya 3 wa Moderna](#) wenye washiriki 30,000, hakuna matatizo hatari ya usalama yalishuhudiwa. Athari zisizokusudiwa zilizoshuhudiwa sana ni uchovu, maumivu ya kichwa, uchungu au kugeuka rangi kwa sehemu iliyodungwa sindano kuwa nyekundu, na maumivu ya misuli au viungo. Athari kama hizi zisizokusudiwa, ingawa hazipendezi, ni ishara kuwa mwili wako unafanya kazi ipasavyo ili kuunda kingamwili dhidi ya virusi vinavyosababisha COVID-19.

Uongo: Chanjo husababisha tawahudi.

UKWELI: Chanjo hazisababishi tawahudi.

Mara kwa mara, tafiti zilizofanyika ulimwenguni kote zinaendelea kuonyesha kuwa [hakuna uhusiano wowote kati ya tawahudi na chanjo.](#)

Ninawezaje kujua ni vyanzo gani vya taarifa za chanjo ya COVID-19 ambavyo ni sahihi?

Inaweza kuwa vigumu kujua ni vyanzo gani vya taarifa unavyoweza kuamini. Intaneti, kwa bahati mbaya, inaweza kuwa na taarifa hatari zisizo sahihi kuhusu chanjo za COVID-19. Jambo bora zaidi unaloweza kufanya ni kujielimisha kuhusu chanjo kwa kutoka kwa taarifa za kuaminika. Jifunze mengi zaidi kuhusu [kupata taarifa za kuaminika za chanjo](#) katika makala haya kutoka CDC katika <https://www.cdc.gov/vaccines/vac-gen/evalwebs.htm>.

Chanzo: [Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa \(CDC\)](#), [Mfumo wa Matibabu wa Chuo Kikuu cha Maryland](#).

Iliundwa tarehe 9 Desemba, 2020

FKwa maelezo zaidi, tembelea coronavirus.ohio.gov.

Kwa majibu ya maswali yako ya COVID-19, piga simu kwa 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634).

Afyako yako ya akili ni muhimu kama ile ya mwili. Ikiwa wewe au unayempenda ana wasiwasi unaohusiana na janga la virusi vya corona, usaidizi unapatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Piga simu kwa Simu ya Usaidizi wa COVID-19 kwa 1-800-720-9616.